

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## BUNGE LA TANZANIA

Simu: +255 026 2322761-5  
Fax No. +255 026 2324218  
E-mail: [cna@bunge.go.tz](mailto:cna@bunge.go.tz)



Ofisi ya Bunge,  
S.L.P. 941,  
**DODOMA.**

### TAARIFA KWA UMMA

Kamati za Kudumu za Bunge zitaanza kukutana Jumatatu tarehe 23 Oktoba 2017 Mjini Dodoma kutekeleza majukumu yake kabla ya kuanza kwa Mkutano wa Tisa wa Bunge tarehe 7 Novemba 2017. Mhe. Spika Job Ndugai ameziita Kamati hizo kuanza shughuli zake tarehe hiyo kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Aidha, Mhe. Spika ameziita Kamati ya Masuala ya UKIMWI, Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) kuanza vikao vyake Oktoba 16, 2017.

Katika kipindi chote hiki, shughuli zilizopangwa kufanyika ni pamoja na kupokea, kuchambua na kujadili taarifa kutoka Serikalini, taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), uchambuzi wa Sheria Ndogo na uchambuzi wa miswada mitatu ya sheria.

Kufuatia Tangazo hili, Wajumbe wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI, Kamati ya mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) wanatakiwa kufika Dodoma tarehe 15 Oktoba, 2017 na Wajumbe wa Kamati nyingine wafike Dodoma tarehe 22, Oktoba 2017. Ratiba ya vikao vya kwa kila Kamati inapatikana katika Tovuti ya Bunge ambayo ni [www.parliament.go.tz](http://www.parliament.go.tz).

Imetolewa na:

Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano  
Ofisi ya Bunge  
S.L.P 941  
**DODOMA**

13 Oktoba 2017